TANGAZO LA SERIKALI NA 531 La Tarehe 21/9/2018

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA

SURA 287

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (UTUNZAJI WA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA ZA MWAKA 2018

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Utunzaji wa Barabara) za Halmashauri ya Wilaya Newala za Mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Newala.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapohitajika vinginevyo:-

"Barabara" Maana yake ni barabara zote zinazopitika kwa magari katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Newala

"Eneo la Barabara" maana yake ni eneo la barabara lililohifadhiwa ambalo ni umbali wa meta kumi na tano (15) kila upande kutoka katikati ya barabara.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya

ya Newala.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

Wajibu wa Halmashauri

4 Ni wajibu wa Halmashauri kuhakikisha kuwa barabara zote zilizo kwenye eneo lake zinapitika majira yote ya mwaka kwa magari ambayo yanakubalika kulingana na uzito.

Marufuku

5 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi:-

(a) kujenga au kulima kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara;

(b) kupitisha wanyama ndani na kando ya barabara;

(c) kufanya biashara ndani ya eneo la barabara.

(d) Kuburuza nondo au vitu vizito barabarani.

(2) Halmashauri itampa notisi ya siku saba (7) mkazi yeyote aliyejenga au kulima kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara ikimtaka mkazi huyo kubomoa jengo lake au kung'oa mazao aliyopanda kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara.

(3) Endapo mhusika atashindwa kutekeleza masharti ya kifungu cha (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kubomoa jengo hilo au kung'oa mazao yaliyopandwa baada ya kupata kibali cha mahakama na kumtaka mhusika kulipa gharama ambazo Halmashauri imeingia.

Makosa

6 Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-

(1) atajenga nyumba au kuchimba mchanga kwenye maeneo ya barabara au hifadhi ya barabara.

(2) ataelekeza maji kwenye maeneo ya barabara.
(3) atapitisha mifugo kwa kuswaga kwenye maeneo ya barabara au hifadhi ya barabara.
(4) ataharibu miundombinu ya barabara.
(5) ataiba alama za barabara.
(6) atakata barabara bila kibali cha Halmashauri.
(7) atatupa takataka kwenye barabara au mitaro pembeni ya barabara.
(8) ataweka tuta kuvuka barabara pasipo idhini ya Halmashauri.
(9) atapitisha gari lenye uzito zaidi ya uwezo wa barabara.
(10) ataburuza nondo,au kitu chochote kizito barabarani.
(11) ataweka kizuizi barabarani

Kufifilisha kosa

7 Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa na kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na kisichozidi shilingi laki tano (500,000) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi, na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

Adhabu

8 Mtu ye yote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja(1,000,000) na kisichopungua shilingi laki mbili (200000/=)au kifungu kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

JEDWALI

Limetungwa chini ya kifungu cha 7

HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi…….. Nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya…….Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Newala kwamba mnamo tarehe…… ya mwezi wa…….mwaka……. nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha …….. Cha Sheria Ndogo hizi za (Utunzaji wa Barabara) Halmashauri ya Wilaya Newala za mwaka 2018, Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa ikiwa Mkurugenzi Mtendaji ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 7 Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe……Sahihi……..……

Mbele yangu;

Jina……

Saini
……

Wadhifa……..…

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Newala uliofanyika mnamo Tarehe 24 Mwezi wa 04 Mwaka 2017 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

MUSSA M. CHIMAE
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya
Newala

L.S

RASHID CHITWANGA. NDEMBO,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya
Newala

NAKUBALI,

Dodoma
27 Agosti, 2018

SELEMANI S.JAFO (MB)
Waziri wa Nchi(-OR TAMISEMI)